

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

KAMPENI YA FURAHA YANGU KUZINDULIWA MKOA WA DAR ES SALAAM

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam **Mhe. Paul Makonda** anapenda kuwakaribisha wananchi wa Mkoa huo kwenye Uzinduzi wa Kampeni ya **FURAHA YANGU** itakayozinduliwa tarehe **07/09/2018** kwenye Viwanja vya **Zakhem Mbagala**.

Kampeni hiyo yenye Kauli Mbiu isemayo **“PIMA, JITAMBUE, ISHI”** inalenga kuongeza Utambuzi wa **VVU** na kuanza Dawa za Kupunguza Makali ya Virusi vya **UKIMWI** Mapema Iwezekanavyo.

Katika Uzinduzi huo Huduma mbalimbali za Afya zitatolewa bila malipo yoyote ambapo kutakuwa na Upimaji wa Virusi vya **UKIMWI**, Uchunguzi wa Saratani ya Mlango wa Kizazi, na Magonjwa yasiyoambukiza. Aidha, wananchi watapata nafasi ya Kuchangia Damu.

Huduma zote hizo zitaanza kutolewa kuanzia tarehe 05/09/2018 hadi tarehe 07/09/2018 kuanzia saa mbili kamili asubuhi.

WITO: Wananchi wote wa Mkoa wa Dar es Salaam tunaombwa kujitokeza kwa wingi **HASA WANAUME** katika Kampeni hii ya **FURAHA YANGU** ili kuzijua vyema Afya zetu.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

04/09/2018

